**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA MBONIMPAYE MPANGO, MKE WA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA SEMINA YA UHAMASISHAJI WA SENSA KWA WANAWAKE 1000 MKOA WA DAR ES SALAAM GOLDEN MEMORY CLASSIC HALL SINZA, DAR ES SALAAM 22 AGOSTI 2022**

**Mheshimiwa Mama Anna Makinda,**

**Ndugu Lilian Wassira, Mkurugenzi wa Taasisi ya Citizens Foundation,**

**Waheshimiwa Wabunge wote mliopo,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**

**Viongozi wa Taasisi mbalimbali mliopo,**

**Wanachama wa Taasisi ya Citizens Foundation,**

**Wageni waalikwa, Akina mama wenzangu,**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

**Kina mama oyee…**

Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa afya njema na kutuwezesha kuwa hapa leo. Nawashukuru sana uongozi wa Taasisi ya Citizens Foundation kwa kunialika hapa nije kushiriki nanyi katika semina hii muhimu ya kuhamasisha wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kuitikia wito wa Serikali wa kushiriki zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ambalo linatarajia kufanyika kesho tarehe 23 Agosti, 2022.

Aidha, napenda pia kukushukuru na kukupongeza Mama yetu Mheshimiwa Anna Makinda, Spika Mstaafu ambaye pia ni Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka huu 2022, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kuhamasisha Watanzania wote kushiriki katika zoezi la sensa. ***Hongera sana mama!***

***Ndugu Viongozi, akina mama wenzangu, na wageni waalikwa***

Ninafurahi na kuhamasika sana ninapoona akina mama wanakuwa mstari wa mbele katika mambo muhimu yanayoigusa jamii yetu. Semina hii ya leo ni muhimu sana kwa manufaa yetu na familia zetu pamoja na taifa kwa ujumla.

Nasema hivi kwa sababu, kama tunavyofahamu, sisi wanawake tunanafasi kubwa sana katika kuhamasisha jamii kutoa ushirikiano wa kutosha ili zoezi la sensa lifanikiwe. Hivyo naamini kupitia semina hii, tutaelimishwa na kupewa miongozo ili na sisi tuweze kuhamasisha wengine katika maeneo yetu tunayoishi au kufanyakazi na kuchangia katika mafanikio ya zoezi hili.

***Ndugu washiriki***

Sensa ya Watu na Makazi ni zoezi la kitaifa na litafanyika kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na miongozo maalum**.** Hivyo naamini kupitia semina hii tutajifunza masuala yote muhimu ambayo yatatuwezesha na sisi kushiriki kikamilifu katika sensa hii. Ni vyema tufahamu kuwa, kupitia Sensa, Serikali inatarajia kukusanya, kuchambua, kutathmini na kutambua takwimu muhimu ikiwemo kujua idadi ya watu wote nchini kwa umri na kwa jinsi, mahali tunapoishi, hali ya elimu, ajira, makazi na pia hali ya vizazi na vifo. Takwimu hizi za Sensa ni msingi wa uandaaji wa Sera na program mbalimbali zinazolenga kuboresha ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa kupitia takwimu hizi Serikali inaweza kuainisha mahitaji ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye mahitaji maalum. Hivyo, nitumie fursa hii kuwasihi sana, kuwepo katika makazi yetu na kutoa ushirikiano wa kutosha ambao ni pamoja na kuwa tayari kutoa taarifa zenu kwa usahihi ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuwa na takwimu sahihi na muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

***Akina mama wenzangu;***

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anadhamira ya dhati kuboresha huduma za kijamii na hasa maisha ya Watanzania kwa ujumla. Tumeona Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa sana kuboresha Sekta ya Elimu, Afya, usafiri na usafirishaji, upatikanaji wa nishati ya Umeme, Kilimo, Viwanda, huduma ya maji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Lakini akina mama wenzangu, ili kufanikisha utoaji sawia wa huduma hizi zote, taarifa zitokanazo na Sensa kwa watu wetu ni muhimu sana katika kuweka mipango na kugawanya rasilimali za nchi kwa maendeleo ya Watanzania.

Hivyo, ni muhimu sana wananchi kuandaliwa ili waweze kushiriki zoezi la Sensa kikamilifu. Naomba nitoe rai kwenu, baada ya semina hii hakikisheni mnatoa elimu juu ya umuhimu wa Sensa, huku mkiwapa wananchi miongozo na utaratibu utakaowezesha kufanikisha zoezi hili kwa ufanisi. Aidha, naomba pia nitoe angalizo kuwa, kila mmoja wetu anapaswa kuhesabiwa mara moja tu kama sheria inavyoelekeza. Naamini, wananchi wakiwa na uelewa watatoa ushirikiano

unaohitajika. Vilevile, Mheshimiwa Rais Samia ametuhakikishia kuwa, taarifa zote zitakazokusanywa wakati wa Sensa zitakuwa ni siri na zitatumika kwa madhumuni ya kitakwimu tu na si vinginevyo, hivyo tusiogope kutoa taarifa sahihi.

***Ndugu Viongozi, akina mama wenzangu, wageni waalikwa***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana wanachama wote wa Taasisi ya Citizens Foundation pamoja na wanawake wengine wajasiriamali hapa nchini kwa kuwa mstari wa mbele katika kutafuta fursa za kujiletea maendeleo na kujikwamua kiuchumi. Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais Samia ni kinara wa utekelezaji wa ajenda ya kumkwamua mwanamke kiuchumi. Mheshimiwa Rais ameahidi kuongeza uwekezaji katika program za elimu kama vile mafunzo ya ufundi stadi na matumizi wa teknolojia kuwaongezea wasichana na wanawake ujuzi ili waweze kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Aidha, katika bajeti yake ya mwaka huu 2022/2023, Serikali imeelekeza Serikali za Mitaa kutenga asimilia 10 ya mapato yake ya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Hali kadhalika, kwa wale ambao wanajishughulisha na sekta ya kilimo, mabenki kadhaa sasa yameanza kutoa mikopo yenye riba nafuu. Hivyo, nitoe rai kwenu kuchangamkia fursa hizi ili tuweze kufikia yale malengo tuliyojiwekea. Aidha, nawaomba Halmashauri zetu, Jukwaa la Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, wanawake na Makundi Maalum kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais yanafanikiwa. Vilevile naomba taasisi za fedha nchini kuunga mkono juhudi hizi za Mheshimiwa Rais na kutanua wigo wa mikopo na kutoa elimu ya biashara kwa akina mama wajasiriamali.

Naomba pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Taasisi ya Citizens Foundation kwa kuwa na program nzuri ya kusaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi mkiamini kuwa Mtoto ni Mama. Nimeguswa sana, hivyo nitumie nafasi hii kuwaomba akina mama wenzangu, viongozi wote mlioko hapa, wadau mbalimbali wa maendeleo na taasisi zote zilizopo hapa kusaidia watoto wetu hawa kutimiza ndoto zao. ***Jukumu hili ni letu sote!***

Baada ya kusema haya machache, naomba nitamke rasmi kuwa Semina ya Uhamasishaji wa Sensa kwa Wanawake 1000 Mkoa wa Dar es Salaam, imefunguliwa rasmi.

***Akina mama oyeee…***

***Sensa…..***

***Asanteni kwa kunisikiliza.***